# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1013

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-780-7

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI KISWAHILI STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023

Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-780-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255-735041168/ +255-735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali .................... iv
Vifupisho .................... v
Shukurani .................... vi
1.0 Utangulizi .................... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu nchini Tanzania .................... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu .................... 1
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu .................... 2
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi .................... 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali, Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 3
    6.1 Mkufunzi .................... 3
    6.2 Mwalimu tarajali .................... 4
    6.3 Mzazi/mlezi .................... 4
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 5
8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 5
9.0 Upimaji .................... 5
10.0 Idadi ya Vipindi .................... 6
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji .................... 6
Mwaka wa Kwanza .................... 7
Mwaka wa Pili .................... 16
Bibliografia .................... 18

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwaka wa Kwanza na wa Pili....3
Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu....6
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza....7
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili....16

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |

## Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule pamoja na wakuza mitaala wa TET.
Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ni la lazima kwa mwalimu anayetarajiwa kufundisha somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III–VI. Lengo la somo hili ni kumwezesha mwalimu tarajali kumudu mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika Elimu ya Msingi Darasa la III–VI. Hivyo, mwalimu tarajali ataweza kupata maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kuwa mbunifu na mnyumbufu katika ufundishaji na ujifunzaji. Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mkufunzi kumwandaa mwalimu tarajali kufundisha somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III–VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Pia, muhtasari utamwezesha mkufunzi kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji zitakazomjengea mwalimu tarajali uwezo wa kufundisha stadi za lugha na kumudu stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake ya ufundishaji na ujifunzaji.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu nchini Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;
(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based research*).

### 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla wa Stashahada ya Ualimu ni:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based action research*).

### 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali umebainishwa katika Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa Mwaka wa Kwanza na wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | 1.1 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusikiliza |
| | 1.2 Kumudu mbinu za kufundisha matamshi |
| | 1.3 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kuzungumza |
| | 1.4 Kumudu mbinu za kufundisha msamiati |
| | 1.5 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusoma |
| | 1.6 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za uandishi |
| | 1.7 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji |
| | 1.8 Kumudu mbinu za kufundisha sarufi ya Kiswahili |
| | 1.9 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali, Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali, mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

**6.2 Mwalimu tarajali**

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ujifunzaji na ufundishaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

**6.3 Mzazi/mlezi**

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika ujifunzaji.

**7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi na jumuishi kumwezesha mwalimu tarajali kumudu mbinu na matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi. Mbinu hizo ni zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kufikiri kitunduizi, kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Mbinu nyingine ni pamoja na majadiliano katika vikundi, igizo dhima, kazimradi, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, changanya kete, utafiti, utunzi wa hadithi, uwasilishaji, masimulizi, michezo mbalimbali na mbinu zingine zinazohusiana kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

Mkufunzi anashauriwa kumwongoza mwalimu tarajali kuwa mbunifu na mnyumbufu katika kutumia mbinu shirikishi wakati wa mazoezi ya ufundishaji na ufaraguzi wa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mazingira halisi ya mwanafunzi.

**8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mkufunzi na mwalimu tarajali wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana mbadala zinazopatikana katika mazingira ya chuoni ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji. Mkufunzi na mwalimu tarajali wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

**9.0 Upimaji**

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia malengo ya elimu yaliyokusudiwa. Upimaji wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili utazingatia upimaji endelevu na tamati ili kutambua uwezo na mahitaji ya ujifunzaji ya mwalimu tarajali. Upimaji huu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Zana zitakazotumika katika upimaji ni zile zitakazozingatia ujenzi wa umahiri kwa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha anampima mwalimu tarajali katika nyanja zote za upimaji ambazo ni maarifa, stadi na mwelekeo. Zana za upimaji zinazoweza kutumika katika ufundishaji na ujifunzaji ni pamoja na; mitihani, majaribio, bungua bongo, mazoezi ya darasani, maswali ya papo kwa papo, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazimradi na nyingine kama hizo ili kuleta ufanisi katika upimaji endelevu wa ujifunzaji wa mwalimu tarajali. Aidha, ni muhimu kufanya upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali ili kubaini kiwango cha ujifunzaji alichofikia katika nyanja zote. Matokeo ya upimaji yatasaidia kufanya uboreshaji ili kuhakikisha malengo ya Elimu ya Ualimu Stashahada ya Elimu Msingi yamefikiwa ipasavyo.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Aidha, mwalimu tarajali atapimwa kwa upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%) na upimaji tamati utachangia asilimia sabini (70%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafaulu, mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli za upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Kiswahili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vitano (5) kwa wiki kwa mwaka wa I na II.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele sita ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

## Mwaka wa Kwanza

**Jedwali Na. 3**: *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | 1.1 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusikiliza | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Kadi za maneno, vibao fumbo, video zenye michezo ya ufundishaji na ujifunzaji stadi za kusikiliza, picha, michoro | 25 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusikiliza zimetumiwa | | |
| | 1.2 Kumudu mbinu za kufundisha matamshi | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno. | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno | Matini za ufundishaji wa matamshi, video zenye maudhui ya matamshi, kadi za maneno, michoro na picha | 25 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno zimetumiwa | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno zimetumiwa | | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa kutamka sauti za herufi mwambatano, silabi na maneno zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kuzungumza | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Matini za kuzungumza, picha, michoro | 28 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kuzungumza zimetumiwa | | |
| | 1.4 Kumudu mbinu za kufundisha msamiati | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Kamusi, kadi za maneno/tungo, vitu halisi, chati za maneno/ tungo, picha na michoro, matini za msamiati | 15 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati zimetumiwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati zimetumiwa | | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa msamiati zimetumiwa | | |
| | 1.5 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusoma | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Matini za kusoma, kadi za maneno/tungo | 28 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai katika kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Mbinu anuai katika kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma zimetumiwa | | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za kusoma zimetumiwa | | |
| | 1.6 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za uandishi | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Matini za kuandika, picha na michoro, kadi za mwaliko na matangazo, chati za miundo mbalimbali ya uandishi | 34 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa zimetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka zimetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi zimetumiwa | | |
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za uandishi zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.7 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji | (a) Kumudu ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | Vifaa saidizi sahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili vimefaraguliwa | Makunzi laini, vitu halisi, video za ufaraguzi na matumizi ya teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji | 20 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | Teknolojia na vifaa vingine saidizi vimetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | | |

## Mwaka wa Pili

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili | 1.8 Kumudu mbinu za kufundisha sarufi ya Kiswahili | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Sanaa na michezo imetumiwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Picha, kadi za maneno/tungo, matini za sarufi, vibao fumbo, mti wa tungo | 125 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Mbinu anuai za kukabiliana na darasa kubwa katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi zimetumiwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi zimetumiwa | | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi zimetumiwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi | Mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa sarufi zimetumiwa | | |
| | 1.9 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa | (a) Kumudu matumizi ya mbinu za usimamizi wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa | Mbinu za usimamizi wa shughuli za ujifunzaji nje ya darasa zimetumiwa | Matini za matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji nje ya darasa, picha na michoro | 50 |

## Bibliografia


Abel, E. M. na Campbell, M. (2009). *Student-centered Learning in an Advanced Social Work Practice Course Outcomes of a Mixed Methods Investigation*. Katika social work education, 28:1 Kur.3-17(2)

Farrant, S. S. (2000). *Principles and practice of education*. Person Education Ltd.

Malawi Institute of Education. (2004). *Participatory teaching and learning: A guide to methods and techniques*. Malawi Institute of Education.

Mtana, N.; Msimbe, A. na Kauki, A. (2003). *Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa maana*. Ecoprint.

Nduguru, S. (1986). *Kanuni na mbinu za kufundisha*. Catholic Publisher.

Quist, D. (2002). *Primary teaching methods*. Macmillan Education.

WyEU. (2005). *Moduli ya somo la ufundishaji*. Wizara ya Elimu na Utamaduni.